*Kioo cha Lugha, Juz. 22(1), 123-136*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i1.8

# Mtindo wa Usambamba katika Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi

*Aloo R. Odhiambo*[1], *Kineene wa Mutiso*[2] *na Kyallo W. Wamitila*[3]

## Ikisiri

Katika makala hii tumechunguza aina mbalimbali za usambamba na mchango wake katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Ili kufanikisha hili, makala imeongozwa na Nadharia ya Umitindo ambayo inachunguza na kutoa fasiri kwa kazi za isimu na fasihi. Nadharia hii imetumika katika makala hii kwa kuwa uchunguzi wa vipengele vya kifasihi hutegemea vile vya kiisimu. Nadharia ya Umitindo inahusishwa na Geoffrey Leech (1969) hasa katika andiko lake la *A Linguistic Guide to English Poetry*. Lengo la uhakiki wetu ni kuweka wazi aina mbalimbali za usambamba zinazobainika katika utenzi huu na michango yake katika kufanikisha fani na maudhui kwenye utungo huu. Kutokana na uchunguzi wetu, tumebainisha kuwa matumizi ya usambamba kama aina ya urudiaji yanachangia katika ukuzaji na uendelezaji wa dhamira, usawiri na ujenzi wa wahusika na kuingiliana na sifa nyingine za kimtindo ili kuibua umbuji wa kijumla wa utungo huu.

## 1.0 Utangulizi

Usambamba ni mbinu ya kifasihi ambayo inahusu kurudiwa kwa maneno yaleyale au vifungu vya maneno mara chache ili wazo liweze kuwa wazi na tena likumbukwe zaidi. Mtunzi anapotumia urudiaji katika tenzi za Kiswahili, basi anafanikisha fani na dhamira katika utenzi huo. Sababu yake ni kwamba mbinu ya urudiaji ni mojawapo ya mbinu ambazo zinatumiwa na mtunzi kuleta mshikamano katika utungo. Urudiaji wa neno au kifungu cha maneno kinachotumiwa na mtunzi wakati mwingine kuongeza msisitizo, kuboresha au kuimarisha ushawishi kuhusu jambo katika utenzi na kuongeza nguvu katika yale yanayozungumziwa. Zaidi ya hayo, urudiaji unaweza kutumiwa kuleta upeo wa utenzi. Matumizi ya urudiaji katika kazi yanaleta ukweli ambao ndio mahitaji ya kimsingi ya

[1] Mwanafunzi wa uzamivu, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: alooronald@gmail.com.

[2] Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: kineenewamutiso@yahoo.com/ mkineene@uonbi.ac.ke.

[3] Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: wamitila@gmail.com

mitindo (Croft na Robert, 2000).

Kwa mujibu wa Fabb (1997) na Jakobson (1983, 1987a, 1987b), usambamba ni sheria kuu ya mitindo katika mawanda na tanzu mbalimbali ya fasihi. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa usambamba ni mlandano wa muundo. Jakobson (1983) anasisitiza kuwa katika usambamba kuna mifumo ya mishabaha katika utungo na kwenye mifuatano ya elementi katika viwango mbalimbali kama vile: mosi, viambajengo vya kisintaksia, uamilifu wa kisarufi na kategoria za kisarufi, usawe wa kileksia na maana za jumla na michanganyiko ya sauti na mpango wa arudhi. Mtindo huu unaleta ulinganifu wa kiuanuwai katika mshororo ambao umeunganishwa kupitia kwa matumizi ya usambamba.

Urudiaji wa kisambamba huwa unatokea wakati sifa mbalimbali za kisambamba kama vile aina ya vishazi, virai au sentensi, vifungu ama beti zinaporudiwa na mtunzi. Urudiaji wa kisambamba ni muhimu kwa sababu unawasaidia wachambuzi katika kutathmini na kutoa maoni juu ya mtindo wa utenzi. Jakobson (1987) anafafanua kuwa usambamba hutokea kwa njia mbalimbali katika utungo. Njia hizi ni pamoja na: kwanza, kunapokuwa na mfanano wa kauli ambapo kile kisemwacho hurudiwa kwa kutumia maneno yanayofanana; pili, kunapokuwa na tabaini ambapo mistari inayoshabihiana inaeleza mkinzano, na mwisho, kunapokuwa na usambamba katika muundo. Msokile (1993) kwa upande wake anaeleza kuwa usambamba unahusu matumizi ya maneno mawili au zaidi au fungu la maneno katika mfuatano maalumu wa kisarufi. Pia, usambamba unatajwa kama mbinu ya kurudia maana fulani kwa muundo mwingine tofauti.

Urudiaji wa kisambamba ni sifa ya kimtindo inayotumiwa ili kuongeza msisitizo na vilevile kuonesha sifa muhimu za utungo kama vile fani na dhamira. Fabb (1977) anaeleza kuwa usambamba una kazi kuu tatu: kwanza, ni kanuni inayofanya utungo kuwa na muundo. Pili, huvuta uzingativu kwenye matini, na tatu, husaidia katika kueleza mtazamo wa kitamaduni juu ya uwili katika dunia. Mwania (2007) anasisitiza kuwa jukumu kuu la usambamba katika ushairi ni kudokeza kwa uwazi kabisa ujumbe ambao msanii anaunuia kwa jamii lengwa. Katika utafiti huu, tunajikita katika kuhakiki jinsi mtunzi alivyotumia urudiaji wa kisambamba ili kufanikisha fani na dhamira mbalimbali kama vile dhamira ya uumbaji, dini, toba, na kadhalika, katika utenzi huu wa *Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

## 2.0 Muhtasari wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*

*Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* (Mhariri, Knappert mwaka wa 1964) una beti mia saba sabini na sita (776). Katika utungo huu, mtunzi anazungumzia masuala mbalimbali kama vile uumbaji ambapo mtunzi anasema kuwa Mungu aliumba vitu vingi ila vinne tu ndivyo vitakatifu. Vitu hivyo vinne ni: malaika (Jiburili, Mikaili, Isirafili na Aziraili); majabali (Jabali Kafu ambalo ni la kheri, Turu, Huda na Arafiya); siku (Lailatu I'Haji, Idi mbili na Laila Miiraji), na hata wanawake (Amina mwana wa Bashira, Mwana Sara ambaye ni mkewe Mtume Ibrahimu, Mariamu bintiye I'Umari ambaye ni mamake Mtume Isa na Saidatina ambaye ni bintiye Shafiina). Vilevile, mtunzi amezungumzia hadithi ya Ali bin Talib anayejibu maswali ishirini ambayo anaulizwa na mgeni Mudhari bin Darimi anayewasili kutoka Meka pindi tu baada ya kifo cha Mtume Muhammad kama njia ya kuzuia maswali mengi kutoka kwa Sheikh Ali kuhusu kifo cha Mtume.

Aidha, maswali haya yanatumiwa kuimarisha imani yake katika dini. Sheikh Ali anathibitisha kuwa anayafahamu maswali haya kwa kutoa majibu yake. Maswali haya, kwa kiwango kikubwa, yana misingi yake katika dini ya Kiislamu. Usimulizi wa Sheikh Ali kuhusu kisa cha Musa na Mariamu ndio unaosisimua zaidi. Hatima ya Mwislamu siku ya kiyama itajikita katika maswali haya (maswali kuhusu uumbaji wa Adamu na Hawa, kuzaliwa kwa Isa pamoja na maisha yake, maswali yanayomhusu Mtume Muhammadi, swali la mawaidha ya Suleimani, maswali kuhusu nguvu za Musa na Firauni, swali la Jabali lililozaa, swali la mbingu na nchi, swali kuhusu jua na mwezi, maswali kuhusu vitu vinavyopendana na vitu visivyopendana, maswali yanayorejelea uelewa wa wema na maovu na swali linalohusu kiungo cha mwili kinachoumbwa wa kwanza baada ya mimba kutungwa). Maswali haya ndiyo nguzo, msingi na mhimili wa dini ya Kiislamu na maisha ambayo Mwislamu anatarajiwa kuishi akiwa hapa duniani.

Pamoja na hayo, kupitia kisa cha mahubiri ya Abu Bakari kuhusu majukumu mbalimbali katika dini ya Kiislamu, mtunzi ametoa wosia kwa Mwislamu kuhusu adhabu atakayopata siku ya kiyama iwapo hataweza kuishi kulingana na sheria za dini yake. Mwislamu anatahadharishwa kuwa atapata adhabu kali kule jahanamu iwapo hatafuata dini. Kwa upande mwingine, Waislamu waliofuata dini wameahidiwa maisha mazuri ya peponi. Isitoshe, wanakumbushwa kuwa dunia hii siyo makao yao kwa vile wao ni wapitanjia tu. Kwa hivyo, ni vyema wajihadhari na anasa za dunia.

**3.0 Misingi ya Nadharia ya Umitindo**

Mtindo unarejelea namna ambavyo mtunzi anatumia lugha yake kulingana na muktadha ili kuwasilisha ujumbe. Kwa mujibu wa Abrams (2015), Nadharia ya Umitindo inachunguza namna ambavyo lugha inatumiwa katika kazi. Nadharia hii ilitokana na Nadharia ya Balagha na kwa sasa inajisimamia na hata kutumiwa katika uhakiki mbalimbali katika ushairi. Geoffrey Leech (1969) ni mtaalamu wa kwanza aliyetumia nadharia hii katika ushairi. Leech (1969) anaeleza kuwa nadharia hii inatumiwa kuhakiki na kutoa fasiri kwa kazi za kifasihi na pia zile za isimu kwa sababu vipengele hivi hutegemeana. Aidha, ni vigumu sana kufafanua na kuainisha vipengele vya kifasihi kama vile urudiaji bila kurejelea vipengele mbalimbali vya kiisimu.

Leech anaendeleza mjadala huu kwa kusisitiza kuwa Nadharia ya Umitindo inasaidia katika kubainisha sheria ambazo zinatumiwa kuteua maneno maalumu katika lugha ambayo inatumiwa kutekeleza shughuli tofautitofauti za kijamii zinazohusisha utoaji na upokezi wa maana ya ujumbe na hata uchanganuzi wa diskosi na fasihi. Katika utunzi wa mashairi, mshairi ana idhini ya kiutunzi ambayo inamwezesha kutumia maneno kwa namna ambayo inabainisha au kudhihirisha urudiaji katika sehemu na viwango tofautitofauti ili kuuwasilisha ujumbe alionao katika utungo wake. Kwa mfano, mtunzi ana idhini ya kutumia anafora (urudiaji wa matumizi ya maneno au virai fulani maalumu kuanza mishororo au mistari mbalimbali ya utenzi wake). Zaidi ya hayo, mtunzi anaweza kutumia epifora (urudiaji wa virai au maneno katika sehemu ya mwisho ya mshororo, virai au sentensi) ili kupitisha ujumbe wake kwenye utungo.

Nadharia ya Umitindo huchunguza kisemwacho na namna kinavyosemwa. Wazo hili linatusaidia katika kuchunguza namna mtunzi anavyotumia urudiaji kama njia ya kufanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Wamitila (2003) anaendeleza mjadala huu kwa kusema kuwa Umitindo ni nadharia inayotumiwa kuchunguza jinsi matukio tofautitofauti yanavyoelezwa katika isimu na fasihi kwa kutumia lugha. Katika makala hii tunachunguza kipengele cha uchimuzi na mtindo. Kipengele hiki kinashughulikia namna ambavyo mtunzi aliichimuza lugha yake kwa kutumia urudiaji wa kisambamba ili kuweka wazi ujumbe wake katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* kama njia ya kufanikisha fani na maudhui kwenye utungo huu.

Baadhi ya mihimili ya Umitindo inayotusaidia katika utafiti wetu ni kama vile: kwanza, ujumbe katika kazi ya kifasihi hutokea katika mtindo wa urudiaji unaohusika. Pili, vipengele vya lugha kama vile mbinu ya urudiaji na ujumbe vina

uhusiano mkubwa na haviwezi vikatenganishwa. Mihimili hii miwili inatusaidia katika kutambua namna ambavyo aina mbalimbali za urudiaji wa kisambamba zimetumiwa na mtunzi. Mwisho, tumebainisha namna ambavyo urudiaji huu wa kisambamba unahusiana na ujumbe na kujenga fani na maudhui.

## 4.0 Uchambuzi wa Data na Matokeo ya Utafiti

Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ametumia aina mbalimbali za urudiaji wa kisambamba katika kuangazia masuala tofautitofauti kwenye utungo wake. Isitoshe, mbinu hii ya urudiaji wa kisambamba ndio msingi wa kuelewa ujumbe wa utenzi huu kuhusu siku ya kiyama na masuala ya uumbaji.

### 4.1 Usambamba wa Kidhamira kuhusu Dini ya Kiislamu

Dhana hii hutumiwa kuelezea urudiaji wa wazo kuu au dhamira ya kazi ya kifasihi. Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, amerudia kwa wingi dhamira kuhusu umuhimu wa kuifuata dini kama muumini wa dini ya Kiislamu. Mambo yanayohusu dini ni masuala muhimu sana ambayo yanasimuliwa katika utenzi huu kama yalivyo katika tenzi mbalimbali za Kiswahili kama vile *Utenzi wa Qiyama*, *Utenzi wa Ngamia na Paa* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Mtunzi wa utungo huu ameyapa nafasi kubwa masuala yanayohusu dini katika kazi yake.

Katika utungo huu, usimulizi wa kisa cha utenzi unaanza kwa sala mahususi kwa Allah (Mungu). Vilevile, anaelezea sababu zake za kutunga na kufafanua kuwa bila maarifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hangeweza kufanikiwa katika kuutunga utungo huu. Mtunzi anaelezea yafuatayo katika sehemu ya kwanza ya usimulizi wake:

> Bismillahi Wahidu,
> Rahamani Li Swamadu,
> Rahimu Rabbu Shahidu,
> Hana kifani Jaliya (ubeti 12).
> Alhamdulillahi,
> Nihimidiye swahihi,
> Niswafiye kulubihi,
> Kwa utakafu wa niya (ubeti 13).

Katika beti hizi, mtunzi anaonesha imani yake katika dini ya Kiislamu kwa kuanza kutoa usimulizi wake kwa kumtaja na kumshukuru Mungu. Vilevile, mtunzi anaelezea baadhi ya sifa za Mungu. Kwa mfano, anafafanua kuwa Mungu ni mkarimu, Mungu ni wa milele na zaidi ya hayo, hana mfanano. Utangulizi huu unaonesha kuwa kisa kinachosimuliwa katika utungo huu ni cha kidini. Fomula hii

ya ufunguzi ni ya kijadi na inapatikana katika tungo mbalimbali za kijadi za aina hii katika fasihi ya Kiswahili kama vile *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Qiyama*. Mtindo huu unatumiwa na mtunzi kama njia ya kumsifu Mungu na Mtume Muhammad. Zaidi ya hayo, mtindo huu wa ufunguzi unatumiwa kama njia ya kuwashauri Waislamu ili wazingatie na tena wafuate sheria na amri za Mwenyezi Mungu pamoja na kumwombea Mtume Muhammad kama njia ya kujiepusha na moto wa jahanamu siku ya kiyama (ubeti wa 11 - 32). Ujumbe uliopo katika fomula funguzi hii unakaririwa mara kadhaa katika utungo mzima (ubeti wa 175):

> Dibaji nimefupiza,
> Kwenda mbee sikuweza,
> Sasa naomba majaza,
> Ya Rabbi nisahiliya (ubeti 175).

Beti za mwisho za utungo huu zinaonesha fomula maalumu ya kufunga. Fomula hii inaonesha njia maalumu ya kutamatisha kisa cha kidini kinachosimuliwa katika utungo huu. Beti hizi za kufunga zinatokea kati ya ubeti wa 772 hadi 776. Katika beti hizi mtunzi anafunga kisa hiki kwa kumwomba Allah (Mungu) amlinde pamoja na familia yake ili wajiepushe na matatizo, maovu na maumivu yaliyo duniani. Isitoshe, mtunzi anamwomba Allah amwepushe na haramu yote ya dunia. Katika sehemu ya mwisho anatuma salamu za heri kwa familia ya Seyidina Ali na kumwomba Mungu awalinde. Kwa mfano:

> La ilaha illa-Llahu,
> La ilaha illa-Llahu,
> La ilaha illa-Llahu,
> Jalla asiyo mithali (ubeti 774).
> Ya Allahu ya Kariimu,
> Ya allahu tukirimu,
> Ya Allahu turahamu,
> Kwa akhira na duniya (ubeti 775).
> Wa Swalla ‘llahu alehi,
> Sayidina wa alihi,
> Wa ala sahabatihi,
> Wa salamu wote pia (ubeti 776).

Beti hizi za mwanzo na mwisho zinazotokea kabla na baada ya usimulizi zinaonesha kuwa utenzi huu umetawaliwa na dhamira ya dini. Suala hili la kidini limetawala katika utenzi wote kutoka mwanzo hadi mwisho. Aidha, suala hili ndilo msingi wa usimulizi wa mambo mbalimbali katika utungo huu. Kama tunavyoona suala hili la dini ndilo linalochangia usambamba wa kidhamira kupitia matumizi ya fomula maalumu za ufunguzi na kufunga katika *Utenzi wa Seyidina*

*Ali na Mudhari bin Darimi*. Fomula hizi zinachangia katika kuendeleza usambamba wa kimuundo. Sababu yake ni kwamba mtunzi ameweza kutumia muundo wa maneno wenye kategoria sawa katika beti tofautitofauti. Mtindo huu unaoonesha kwamba usambamba wa kidhamira pia unapatikana katika tungo mbalimbali za kijadi za aina hii katika fasihi ya Kiswahili kama vile *Utenzi wa Qiyama*.

Usambamba wa kidhamira unaohusu dini ambao unatokea katika utenzi huu unachangia katika ukuaji wa mandhari na mahali katika kazi hii. Mandhari katika utungo huu ni ya Kiislamu. Mandhari haya yametumiwa kuwatambulisha wahusika wakuu mbalimbali katika kazi hii kama vile Allah, Mtume, Sheikh Ali na Seyidina Ali. Wahusika hawa ni muhimu kwa kuwa ndio wanaoshiriki katika kutekeleza shughuli mbalimbali katika utenzi huu. Aidha, dhamira ya imani na dini zinawasilishwa kupitia wahusika hawa. Mwisho, usambamba wa kidhamira katika utungo huu umeoneshwa kupitia urudiaji wa masuala mbalimbali kama vile hukumu, toba, uumbaji na kifo. Masuala haya yamesheheni katika utungo wote.

### 4.2 Usambamba wa Kisintaksia

Usambamba wa kisintaksia ni urudiaji ambao unahusu kurudiwa kwa miundo ya kisintaksia. Usambamba huu unatokea pale ambapo miundo ya sentensi na vipengele mbalimbali vinavyounda sentensi kama vile maneno na vifungu vinarudiwa. Kwa kuzingatia kanuni zinazohusu kurudiwa kwa sentensi, usambamba wa kisintaksia unahusisha uchunguzi wa namna sentensi mbalimbali zinavyoundwa. Kauli hii inaleta maana kuwa miundo tofautitofauti ya kisintaksia inaweza kutokea katika mstari fulani wa utungo na ukarudiwa katika mstari au kifungu hichohicho kwa kuchukua nafasi sawa. Zaidi ya hayo, sehemu ambapo miundo fulani imedondolewa, msomaji au wasomaji wanaweza kuitia akilini wakati wanaposoma. Miundo hii ambayo imedondolewa huweza kurudiwa katika nafasi sawa kama njia ya kujiepusha na uziada katika kazi. Mtunzi wa utungo hutumia usambamba wa kisintaksia kama njia ya kusisitiza ujumbe ambao unawasilishwa kwa namna ya kipekee bila kutokea kwa uziada wa muundo unaohusika.

Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* mtunzi ameweza kutumia usambamba wa kisintaksia kwa wingi. Mifano ni kama ifuatayo: *Aketiyo na ghanii*, *aketiyo na kijana*, *aketio na fukara*, *aketio na salihi* na *aketio na alimu* (beti za 660 – 664).

> **Aketiyo na ghanii**,
> Humpa Mola abai,

Ya pupa na utumai,
Na mali kutowekeya (ubeti wa 660).
**Aketiyo na kijana**,
Humzidiya Rabbana,
Pumbao kuu tanena,
Na matezo na ghasiya (ubeti wa 661).

Katika mfano huu, mtunzi ametumia muundo sambamba wa kisintaksia. Matumizi ya usambamba wa kisintaksia katika utungo huu yanasaidia katika kujenga ruwaza ya aina fulani ya kishairi. Matumizi ya usambamba huu yanasaidia katika mijalizo ya kifafanuzi ya sifa za anayewasaidia watu mbalimbali wanaopitia hali tofautitofauti. Urudiaji huu wa kisambamba unatokea katika beti tano lakini kwa mabadiliko ya maneno. Katika urudiaji wa mistari hii, mtunzi anazungumzia sifa za watu wanaopendwa zaidi na Mungu. Anasisitiza kwamba Mungu anawapenda watu wanaowashughulikia watu wenye matatizo mbalimbali katika jamii kama vile: wapotovu, mafukara, salihi, na kadhalika. Aidha, anaeleza kwamba watu wanaowashughulikia watu hawa huwa wanabarikiwa zaidi na Mungu na maisha yao hujaa mafanikio.

Zaidi ya hayo, urudiaji huu wenye usambamba wa kisintaksia unachangia katika kuonesha sifa za ukarimu, ucha Mungu, upole na utiifu, za wahusika mbalimbali kama vile Mtume Muhammad, Ali, Isa, Mudhari bin Darimi, Seyidina Ali na Waislamu wanaopatikana kwenye utungo huu. Vilevile, dhamira ya ukarimu na upendo zinaendelezwa na mtunzi kupitia urudiaji huu wenye usambamba wa kisintaksia. Urudiaji wa mistari hii pia unaleta msisitizo wa ujumbe kwani ujumbe huu unakumbukika kwa muda mrefu na msomaji.

### 4.3 Usambamba wa Kiwizani

Usambamba wa kiwizani ni aina ya urudiaji unaohusishwa na kurudiwa kwa mifuatano ya mapigo ya sauti au ruwaza ya sauti na urudiaji wa beti au kifungu. Katika usambamba huu, urudiaji ambao unatumiwa unasaidia katika ujenzi wa wizani wakati ruwaza fulani ya sauti hukaririwa huku kifungu kirefu na kifupi au sentensi ndefu na fupi zikibadilishwa. Mipangilio hii maalumu ambayo inarudiwa ndiyo inaleta mapigo.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa dhana ya usambamba wa kiwizani hutumiwa ili kutoa maelezo kuhusu ruwaza fulani inayorudiwa huku ikiakisi mwendo wa usimulizi. Sababu yake ni kwamba wizani hurejelea mapigo maalumu yanayoletwa na matumizi ya ruwaza fulani katika ushairi. Vilevile, Wamitila (2008) anatoa maelezo zaidi kwa kusisitiza kwamba usambamba wa kiwizani huweza kuhusishwa na mashairi hasa yale yanayozingatia mapigo maalumu baada

ya kipindi fulani. Isitoshe, anafafanua kuwa shairi lolote huwa na mapigo hayo lakini mapigo hutokea kwa uwazi zaidi katika shairi la kijadi. Mathalani, utungo wa kijadi huwa na idadi maalumu ya mizani ambayo imepangwa katika vipande vilivyo na urefu maalumu na vyenye mpangilio maalumu ambao ni msingi wa usambamba wa kiwizani.

Matumizi ya usambamba wa kiwizani ni sifa ya utanzu wa ushairi kwa sababu utanzu huu hukuza aina hiyo ya wizani. Mtindo huu wa usambamba wa kiwizani umetumiwa kwa wingi sana katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Sababu yake ni kwamba kuna matumizi ya mbinu za kiarudhi katika utenzi wenyewe hususani kuwapo kwa mizani na vina na urudiaji wa kileksia (wa maneno mahususi) kama nguzo ya ujenzi wa usambamba wa wizani. Kwa mfano:

Mambo haya ya Alii,
Wa kuyuwa ni Nabii,
Amma ni wake waswii,
Nawe takubainiya (ubeti 217).
Hapo Abali Hasani,
Akamwambiya mgeni,
Nguo funuwa usoni,
Nataka kwangaliya (ubeti 218).
Alii bin Talibu,
Upesi akamjibu,
Atakao matulubu,
Usiikhini nambia (ubeti 220).

Katika beti hizi tatu, mtunzi ametumia mpangilio maalumu wa mizani. Beti zote zina mizani nane katika kila mshororo au mstari. Aidha, silabi za mwisho katika mishororo ya beti hizi zinaishia kwa sauti maalumu. Mishororo mitatu ya kwanza katika ubeti wa 217 inaishia na silabi **i,** huku mishororo mitatu ya kwanza katika ubeti wa 218 ikiishia na silabi **ni**. Vilevile, mishororo mitatu ya kwanza katika ubeti wa 220 inaishia na silabi **bu**. Muundo huu wa usambamba wa kiwizani ambao tumeonesha katika mifano hii michache unatokea katika beti zote za utenzi huu.

Katika beti tulizotaja hapo juu, mtunzi ametumia usambamba wa kiwizani ili kuleta ujumbe wa kumtambulisha mgeni Mudhari bin Darimi kwa Sheikh Ali aliyewasili Meka baada ya kifo cha Mtume Muhammad. Mgeni huyu anamuuliza Sheikh Ali maswali kama njia ya kumzuia ili asiulize maswali yanayohusu kifo cha Mtume. Aidha, maswali haya yote yanajibiwa na Sheikh Ali. Katika beti hizi mtunzi anaendeleza dhamira ya kifo ambayo imetokea kwa wingi katika utungo huu.

Katika utungo huu mtunzi ameakisi usambamba wa kiwizani kama njia ya kuwavuta wasomaji katika utenzi wake. Sababu yake ni kwamba mtindo huu ambao umetumiwa na mtunzi unafanya sura ya kazi hii kupendeza, na vilevile, *umeleta* mapigo na midundo ya kimuziki katika utenzi huu. Mtindo huu wa usambamba wa kiwizani umetumiwa kama njia ya kuendeleza dhamira ya kidini, sala na toba ili Mwislamu ajiepushe na moto wa jahanamu siku ya kiyama. Mifano hii ni ithibati ya madai yetu:

Basi ndiye tuombao,
Moto twepukane nao,
Shetani na wandamao,
Wataiona hawia (ubeti wa 135B).
Nao ni hao kafiri,
Wakafa wasiyakiri,
Motoni wamehitari,
Watiwa kuikalia (ubeti wa 135C).

Zaidi ya hayo, mtunzi anamshauri Mwislamu amwombe Mungu kila wakati ili ajiepushe na adhabu ya moto itakayotokea siku ya kiyama. Mtunzi anasisitiza kuwa Waislamu wanapoomba basi watajiepusha na matendo ya kishetani. Isitoshe, mtunzi anaelezea kuwa matendo haya ya kishetani huwa yanahusishwa tu na kafiri.

### 4.4 Usambamba wa Kimuundo

Usambamba wa kimuundo ni ule ambao unahusisha kurudiwa kwa ruwaza ambayo ina miundo sawa, kurudiwa kwa miundo ya sentensi na elementi mbalimbali za sentensi kama vile maneno na kishazi. Usambamba huu hubainika wakati ambapo mtunzi anarudia miundo inayofanana yenye kategoria ya maneno ambayo inafanana na wakati mwingine kutokea mahali sawa au ileile. Katika usambamba huu, mtunzi huwa anatilia mkazo zaidi katika urudiaji wa ruwaza unaohusisha miundo ambayo ni sawa. Katika utungo wetu, mtunzi ametunga beti mbalimbali zenye miundo sawa. Mathalani:

Aketiyo na ghanii,
Humpa Mola abai,
Ya pupa na utumai,
Na mali kutowekeya (ubeti wa 660).
Aketiyo na kijana,
Humzidiya Rabbana,
Pumbao kuu tanena,
Na matezo na ghasiya (ubeti wa 661).

Katika mfano huu, mtunzi ametumia muundo sambamba wa kisintaksia. Katika urudiaji wa mistari hii, mtunzi anazungumzia sifa za watu wanaopendwa zaidi na

Mungu. Anasisitiza kwamba Mungu anawapenda watu wanaowashughulikia watu wenye matatizo mbalimbali katika jamii kama vile: wapotovu, mafukara, salihi, na kadhalika. Aidha, anaelezea kwamba watu wanaowashughulikia watu hawa huwa wanabarikiwa zaidi na Mungu na maisha yao hujaa mafanikio. Mifano hii ya usambamba wa kimuundo inasaidia katika kuendeleza dhamira ya utu na utiifu katika utungo huu.

**4.5 Usambamba wa Kifonolojia**

Usambamba wa kifonolojia hutokea pale ambapo mtunzi anarudia sauti fulani maalumu katika utungo wake. Usambamba huu mara nyingi hutokea katika viwango vya irabu au konsonanti. Isitoshe, usambamba wa aina hii unaweza kujitokeza kutokana na matokeo ya miundo ya lugha yenyewe. Ngonyani (2005) anafafanua kuwa usambamba wa kifonolojia hutokea katika ruwaza ambazo zinahusu sauti, toni, kiini-toni, kiimbo, mkazo na mpangilio wa silabi. Urudiaji wa sauti au silabi fulani hupambanua utungo. Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* mtunzi amerudia sauti mbalimbali na mpangilio wa silabi. Mifano ni kama ifuatayo:

> Kitupa cha zinjefuri,
> Niwekeani tayari,
> **Zikome ziwe zizuri,**
> Zipendeze kwangaliya (ubeti wa 4).
> **Ya Allahu** ya Kariimu,
> **Ya Allahu** tukirimu,
> **Ya Allahu** turahamu,
> Kwa akhira na duniya (ubeti 775).

Katika mifano hii, mtunzi amerudia silabi **zi**, **ya**, **la**, **hu** na **a**. Urudiaji wa silabi hizi unasaidia katika kuleta mdundo maalumu na mirindimo katika utungo huu. Zaidi ya hayo, ni sauti ambazo zimetumiwa na mtunzi ili kupitisha ujumbe wa utenzi kwa midundo maalumu. Kupitia matumizi ya silabi hizi, mtunzi ameweza kupitisha ujumbe ambao unakumbukika kwa haraka na urahisi. Aidha, mbinu hii inamsaidia mtunzi katika kuendeleza dhamira ya dini ya Kiislamu.

Katika ubeti wa 775, mtunzi ametumia usambamba wa kifonolojia wakati maneno **Ya Allahu** yanaporudiwa katika mishororo mitatu ya kwanza kama njia ya kusisitiza kuwa ni Mungu. Sababu yake ni kwamba maisha yetu yanategemea msamaha wa Mungu na maelekezo yake. Mfano huu unafungamanishwa na fomula maalumu za kidini za kufunga.

### 4.6 Usambamba wa Kimandhari

Usambamba huu unahusu kurudiwa kwa mazingira fulani maalumu au mazingira ambayo yanakaribia kufanana. Mathalani, *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ni utungo ambao umesheheni kurudiwa kwa mazingira tofautitofauti. Katika urudiaji huu unaohusu usambamba wa kimazingira, mandhari ya peponi na jahanamu yanafafanuliwa na mtunzi kama ifuatavyo:

Akhusu tumwa Amini,
Ateuwe wa peponi,
Na ambao mbwa motoni,
Hana budi na kungiya (ubeti wa 141).
Isimu hwitwa Hashiri,
Atatwandama Bashiri,
Siku nyuma yenye hari,
Tutakapofunguliwa. (ubeti wa 143)
Siku ya ndaa na nyota,
Na adhabu na matata,
Mtume atatwangata,
Kama wene wa kuzaa (ubeti wa 144).

Katika ubeti wa 141, 143 na 144 mtunzi anatuelezea mandhari ya peponi na jehanamu. Mtunzi anasisitiza kuwa watakaoenda peponi ni wale Waislamu walioamini na kuyafuata maneno ya Mtume Muhammad. Mtunzi anatukumbusha kuwa hii ni siku ya njaa na joto, yaani siku ya hukumu au siku ya kiyama au siku ya kwenda peponi na jahanamu ambapo watu wataadhibiwa vilivyo. Vilevile, adhabu watakazopata waja zitategemea matendo yao ya hapo awali.

Katika beti za 640–653, mtunzi anarudia mandhari haya ya peponi kwa kusimulia kisa cha kwenda peponi siku ya kiyama. Anasisitiza kuwa watakaoenda peponi ni watu wakarimu pekee. Aidha, anawatahadharisha Waislamu kuwa waliokaidi amri za Mola wataumia na kuangamia siku hii. Kwa hivyo, ni heri kutenda mema kuliko kutenda maovu. Usambamba wa kimandhari katika utungo huu unasaidia katika kujenga na kuimarisha dhamira za utungo huu.

Kwa ujumla, matumizi ya usambamba wa kimandhari yanaleta mazingira na mandhari ya peponi yaliyorudiwa na mtunzi. Mazingira na mandhari haya ya peponi yanaonesha watu walionawiri, wenye raha, watukufu, wanaosifu na kutukuza jina lake Mungu. Kwa upande wa pili, kuna mandhari na mazingira ya jahanamu ambayo ni ya kutisha na kuogofya. Katika mandhari haya ya jahanamu, kuna watu waliodhoofika kiafya kutokana na kuchomwa kwa moto na kuliwa na majoka. Aidha, ni mandhari yenye vilio na giza tororo. Hebu tuangalie hayo katika beti zifuatazo:

Na pepo ndangu Latifu,
Maulana Ashrafu,
Utwambiziye Sharifu,
Umati yangu sikiya (ubeti 640).
Na twaa ndenu yuwani,
Sute mbwakufa twaani,
Waja tungiye peponi,
Tutiipo tutangiya (ubeti 641).

Matukio mbalimbali yamesimuliwa na mtunzi kutokana na usambamba huu wa kimandhari, kwa mfano: watu kuchomwa motoni, watu wanaosherehekea na kuabudu na watu wanaolia na kulalama. Vilevile, wahusika wengine wakuu kwa wadogo wametambulishwa katika usambamba huu. Wahusika ambao wametambulishwa na mtunzi ni kama vile: Malaika Jiburili, Makafiri, na Watukufu (Waislamu). Wahusika Mtume na Mungu pia wamezidi kutajwa na sifa zao kufafanuliwa. Dhamira ya toba inatokea katika usambamba huu wakati ambapo Waislamu wanahimizwa watubu na watende mema ili waweze kujiepusha na moto na maangamio kule jahanamu.

**5.0 Hitimisho**

Katika makala hii tumeangazia namna ambavyo urudiaji wa kisambamba unachangia katika ukuaji wa fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Katika uhakiki huu, tumedhihirisha jinsi mtunzi alivyotumia aina mbalimbali za urudiaji wa kisambamba. Aina hizi za usambamba ni pamoja na: usambamba wa kidhamira, usambamba wa kisintaksia, usambamba wa kiwizani, usambamba wa kimuundo, usambamba wa kifonolojia na usambamba wa kimandhari. Kwa mfano, mtunzi anapotumia usambamba wa kimuundo, anarudia muundo unaoonesha uwezo wake wa kutumia mtindo huu katika kuendeleza dini ya Kiislamu. Vilevile, kupitia mbinu hii ya urudiaji wa kisambamba, tabia na sifa za wahusika tofautitofauti zinakuzwa kutokana na matendo na shughuli zao za kila siku katika dini ya Kiislamu. Isitoshe, urudiaji huu wa kisambamba umekuwa na umuhimu katika kuleta mwangwi wa kidhamira na usisitizaji. Mwisho, tumeonesha athari ya mbinu hii ya urudiaji wa kisambamba katika uwasilishaji wa maana.

**Marejeleo**

Abrams, M.H. (2015). *A Glossary of Literary Terms*. New York: Cengage Learning, Inc.

de Beaugrande, R.A. na Dressler, W.U. (1981). *Introduction to Text Linguistics*. London: Longman, Inc.

Croft, S. na Robert, M. (2000). *Exploring Language of Literature*. London: Oxford University Press.

Fabb, N. (1977). *Linguistics and Literature*. Oxford: Blackwell Publishers.

Jakobson, R. (1983). *Dialogues*. Cambridge, Mass: Massachusetts Institute of Technology.

Jakobson, R. (1987a). "Grammatical Parallelism and its Russian Facet." Katika K. Pomorska na R. Stephen (Wah,). *Language and Literature*. Cambridge, Mass: Belknap Press of Harvard University University Press. Kur. 145 – 179.

Jakobson, R. (1987b). "Linguistics and Poetry." Katika K. Pomorska na R. Stephen (Wah,). *Language and Literature*. Cambridge, Mass: Belknap Press of Harvard University University Press. Kur. 62 – 94.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ngonyani, D. (2005). "Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii." *Swahili Forum*. 12: 121 – 132.

Mwania, J.M. (2007). "Usambamba katika Ushairi-Huru." Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi* l: *Msingi wa Uchanganuzi wa Kiswahili wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Ltd.